BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Thelathini na Mbili – Tarehe 27 Juni, 2024

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa

1. Ukaguzi wa Kiufundi wa Ukarabati wa Uwanja wa Michezo Gombani Chake Chake Pemba, kwa Kipindi cha Mwaka wa fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2023.

2. Ukaguzi wa Mifumo ya Tehama kwa Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2023.

3. Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Tawala za Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2023.

4. Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi wa Hospitali Kumi za Wilaya na Hospitali Moja ya Mkoa kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2023.

5. Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha Unaoishia tarehe 30 Juni, 2023.

6. Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2023.

7. Ukaguzi wa Kiufundi wa Mradi wa Usambazaji wa Miundombinu ya Maji Safi na Salama, Unguja na Pemba kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2023.

8. Ukaguzi wa Mashirika ya Umma na Taasisi Zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2023.

**Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo na mambo mengine yanayohusiana nayo.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC):**

1. Ukaguzi wa Kiufundi wa Ukarabati wa Uwanja wa Michezo Gombani Chake Chake Pemba, kwa Kipindi cha Mwaka wa fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2023.

2. Ukaguzi wa Mifumo ya Tehama kwa Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2023.

3. Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Tawala za Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2023.

4. Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi wa Hospitali Kumi za Wilaya na Hospitali Moja ya Mkoa kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2023.

5. Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha Unaoishia tarehe 30 Juni, 2023.

6. Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2023.

7. Ukaguzi wa Kiufundi wa Mradi wa Usambazaji wa Miundombinu ya Maji Safi na Salama, Unguja na Pemba kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2023.

8. Ukaguzi wa Mashirika ya Umma na Taasisi Zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2023.

## III. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

267. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuzijenga Ofisi za Mkuu wa Mkoa zinazoendana na hadhi zao.

282. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Messi ya Dunga, Messi ya Ubago ni sehemu za starehe zinazopiga mziki kwa sauti kubwa usiku, kiasi ya kuwakera wananchi wa maeneo ya Ubago, Kidimni na hata Dunga.

(a) Je, kupiga mziki kwa sauti kubwa katika Messi hizo, kunakubaliwa kwa utaratibu upi.

(b) Katika sehemu za starehe zenye kukiuka maadili ya Kizanzibari ikiwa ni pamoja na kuenea kwa vitendo vya ukahaba na matumizi ya vilevi ni pamoja na Messi ya Dunga na Ubago, je, kwa kiwango gani Serikali imefanya tathmini ya kuharibika kimaadili kwa vijana wake wanaofika katika Messi hizo.

(c) Je, Serikali inanufaika vipi na uwepo wa Messi hizo.

### Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

138. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Pamoja na kuongezeka kwa huduma za kibenki hapa Zanzibar, bado zipo benki nyingi ambazo hazina matawi yake hapa Zanzibar, hali inayopelekea wahitaji wa huduma zao kuzifuata Tanzania Bara. Jambo hili limeleta changamoto nyingi kwa wananchi waliopo katika visiwa vya Unguja na Pemba hasa tukizingatia ukuwaji wa utalii na uwekezaji katika visiwa vyetu.

(a) Je, ni benki ngapi ambazo zimepewa leseni na Benki Kuu ya Tanzania (BOT) ambazo hazitoi huduma Zanzibar.

(c) Je, kanuni na sheria za Benki Kuu ya Tanzania (BOT) zinazungumzia vipi juu ya benki hizi kuwa na matawi yake hapa Zanzibar.

(c) Je, Serikali inachukua jitihada gani kuwarahisishia wananchi hawa wanaohitaji huduma za benki hizi.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

219. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kwa kiasi gani harakati za binaadamu zinachangia kuharibu rutuba ya asili ya ardhi yetu, jambo ambalo linatupelekea kutumia mbolea za ziada kwa kiwango kikubwa.

230. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Je, tathmini ya utekelezaji wa haki za wanyama pamoja na uelewa wa haki za wanyama uko vipi katika jamii yetu.

**Wizara ya Afya:**

291. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwenye hospitali zetu wako madaktari dhamana pamoja na makatibu wa hospitali.

(a) Je, ni yepi majukumu yao na wao wanawajibika kwa nani.

(b) Je, majukumu ya Mkurugenzi Tiba na maafisa wake waliopo Unguja na Pemba ni yepi wakati kampuni zilizopo ndio zinaendesha utawala wa hospitali hizo.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

273. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kumekuwa na ongezeko kubwa la shughuli za kijamii zinazofanyika katika kumbi binafsi na za kukodi. Hata hivyo, wimbi la shughuli zinazokiuka maadili na silka za Wazanzibari limekuwa kubwa na likiongezeka siku hadi siku.

(a) Je, kwa kiasi gani Serikali imekuwa ikifuatilia vibali vya shughuli katika kumbi mbali mbali nchini, ili kuhakikisha kwamba shughuli hizo haziendi kinyume na maadili na utamaduni wa Wazanzibari.

(b) Kwa kuwa zipo baadhi ya kumbi kama Ukumbi wa Royal wa Mikunguni na nyumba za watu binafsi ambamo mara nyingi kunashuhudiwa kufanyika kwa shughuli za kusherehekea kuzaliwa ama harusi, huku wahusika wakuu wakiwa watu wa jinsia ya kati na wengi wa wanawake wakiwa na mavazi yanayokiuka maadili na silka za kizanzibari, Je, jambo hili linachukuliwa vipi na Serikali.

(c) Je, ni hatua gani za kinidhamu na kisheria Serikali imewahi kuzichukua kwa matendo kama hayo.

## IV. HOJA ZA KAMATI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo:**

Azimio la Marekebisho ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020.

## V. KAULI ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Hotuba za Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa:

1. Ukaguzi wa Kiufundi wa Ukarabati wa Uwanja wa Michezo Gombani Chake Chake Pemba, kwa Kipindi cha Mwaka wa fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2023.

2. Ukaguzi wa Mifumo ya Tehama kwa Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2023.

3. Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Tawala za Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2023.

4. Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi wa Hospitali Kumi za Wilaya na Hospitali Moja ya Mkoa kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2023.

5. Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha Unaoishia tarehe 30 Juni, 2023.

6. Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2023.

7. Ukaguzi wa Kiufundi wa Mradi wa Usambazaji wa Miundombinu ya Maji Safi na Salama, Unguja na Pemba kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2023.

8. Ukaguzi wa Mashirika ya Umma na Taasisi Zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2023.

## VI. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo na mambo mengine yanayohusiana nayo – Kusomwa kwa Mara ya Kwanza.

**Zanzibar,**
**27 Juni, 2024.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA**